

## **Muda wa Hatua!**

Washiriki watajifunza jinsi ya kukuza mpango wa kwanza kwa kampeni zao binafsi za utetezi.

## **Nyenzo**

Kitini cha Kampeni ya Utetezi

# **Mpango wa Mabadiliko!**

## **Sehemu ya Kwanza**

### **Ambia Wanafunzi Wako**

Katika tajiriba nyingine ya mafunzo iliyounganishwa na ushiriki wa kiraia na kisiasa ambayo tumeyakamilisha pamoja, tulichunguza maarifa na hoja tofauti zinazoweza kuwa na umuhimu kwa kuwa watetezi wa mabadiliko.

Tumetambua masuala yanayoathiri jumuiya zako na kujifunza kuhusu zana maalum za utandaaji na midia ili kutekeleza mabadiliko chanya.

Sasa, ni wakati wa kuleta hoja hizi pamoja na kupanga kampeni yako mwenyewe ya utetezi kutoka mwanzo hadi mwisho!

### **Mwingiliano wa Darasa**

Kwa hiari: Wasilisha kampeni ya sasa na ya utetezi muhimu wa vijana inayoambatana na muktadha wako / eneo la ndani la mshirika / kimaeneo. Tovuti Voices of Youth (katika Kiingereza, Kihispania, Kifaransa, na Kiarabu) na Global Voices (iwapo ina manufaa, ndani ya tovuti, tafuta neno "kijana") linaweza kutumika kama vyanzo vya uhamasisho iwapo huna uhakika kuhusu kampeni ya kuteua. Kuwa huru kuonyesha tovuti ya kampeni kwenye kiwambo unavyoifafanua.

# Kazi

## Kazi

### Ambia Wanafunzi Wako

Unda maandishi yanayofupisha kampeni ya utetezi ambayo ungependa kuendesha kwenye jumuiya yako. Unaweza kujumuisha matini uliyoyaandika kwenye baadhi ya tajiriba ya awali ya mafunzo. Kwa mfano, unaweza kushirikisha maelezo kuhusu suala ambalo unataka kulizungumzia, au ufafanuzi kuhusu ni kwa nini mwigizaji wa utamaduni wa upeushaji uliochagua kwa kampeni yako unavyoambatana na malengo yako ya utetezi. Utakuwa na dakika 30 za kubuni kampeni yako.

Tafadhali jibu maswali yafuatayo:

1. Je, ungependa kuzungumzia suala lipi?
2. Je, hii inaathiri jumuiya gani?
3. Ungependa kuzungumzia suala hili kiviipi?
4. Ni majukwaa gani ya midia utakayoyatumia ili kuibua uhamasisho kwenye sababu yako? Kwa njia zipi?
5. Je, kuna mwigizaji wa utamaduni wa upeushaji ungependa kutumia kwa kampeni yako? Kiviipi?
6. Ni nani atakayekuwa kwenye mtandao wako wa auni?
7. Ni alama ipi ya reli ungependa kuunda kwa kampeni yako?
8. Je, kalenda ya matukio ya kampeni yako ni ipi?

Jihisi huru kukuza hoja zako kuhusu Lahakazi la Kampeni ya Utetezi, au kwenye karatasi tofauti.

### Utoaji

Pitisha Lahakazi la Kampeni ya Utetezi kwa washiriki.

### Mwingiliano wa Darasa

Sasa, mkiwa katika jozi, mtashiriki maandishi yenyu ya kampeni ya utetezi. Zungumza na mshirika wako kuhusu kigezo cha kampeni yako ambacho umefurahia zaidi kukihusu.

## **Mwingiliano wa Darasa**

Waruhusu washiriki wachukue dakika 20 ili kushiriki kampeni yao kwenye jozi.